# Siku ya Mazingira <u>yafana</u> Wilayani Karagwe

**INNOCENT E. MWALO.**

Maadhimisho ya siku ya Mazingira Duniani ambayo huadhimishwa kila tarehe 5 Juni, ya kila mwaka siku ambayo watanzania huungana na mataifa mengine duniani kuadhimisha siku hii adhimu wilayani Karagwe mwaka huu yalifanyika katika kijiji cha Omkakajinja kilichopo katika kata ya Rugera huku Mgeni rasmi akiwa Katibu Tawala wa Wilaya hii, ndugu Innocent Nsena aliyekuwa anamwakilisha Mkuu wa Wilaya Karagwe ambapo kwa mwaka huu maadhimisho haya yanaonekana kufana sana.

Awali kabla ya shughuli za maadhimisho hayo kuanza burudani za ngoma zilitumbuiza halaiki hiyo iliyokuwa imekusanyika kufuatilia maadhimisho hayo huku maada mbalimbali zilizokuwa zimeandaliwa kwa ajili ya kuhasisha wananchi juu ya uhifadhi wa mazingira zikitolewa.

Madhumuni ya maadhimisho ya siku hii ya mazingira duniani ni kuhamasisha jamii duniani kote kuelewa masuala yahusuyo mazingira na pia kuhamasisha watu wa jamii mbalimbali duniani kuwa mstari wa mbele katika kuchukua hatua za kuhifadhi na kulinda mazingira ambapo wilaya ya Karagwe kama sehemu nyingine zenye changamoto ya mazingira maadhimisho haya yalikuwa ni muhimu kwa ajili ya Elimu ya mazingira.

Kwa upande wa wananchi wa Karagwe maadhimisho haya yalitumika kama fursa kwa jamii hii kufahamu wajibu wao wa kuzuia madhara na mabadiliko hasi katika mazingira na kuhamasishwa kama jamii kufanya mazingira yao kuwa salama na masafi i kwa ajili kufurahia hali hiyo katika maisha ya sasa na ya vizazi baadae.

Mgeni rasmi, katika salamu zake alitumia maadhimisho hayo kutoa maagizo ya serikali ya kuwasisitiza wananchi wa wilaya ya Karagwe kutunza vyanzo vya maji na kuepuka kuchoma miti ovyo kwa ajili ya kulinda mazingira.

"Napenda kutumia fursa kuwapa taarifa kuwa kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya itafanya ukaguzi kuanzia tarehe mosi mwezi wa saba mwaka huu katika maeneo yote ya wilaya Karagwe ili kubaini kama kuna vyanzo

vya maji vimeharibiwa kwenye maeneo hayo na hatua kali zitachukuliwa dhidi ya yeyote atakayeonekana kukiuka maaagizo hayo", alisema Katibu Tawala huyo.

Kwa upande wake Makamu Mwenyekiti wa Halamashauri ya Wilaya hii Mheshimiwa Dauson Paulo Byamanyirohi ambaye pia ni Diwani wa kata ya Rugera aliiambia hadhara hiyo kuwa Kaulimbiu inayoongoza maadhimisho ni hayo ni : "Mahusiano Endelevu Kati ya Binadamu na Mazingira".

Ambapo kwake Kaulimbiu hii inawahamasisha wananchi kuwa na urafiki endelevu na mazingira asilia ambapo kila mtu anapaswa kutambua, kufurahi, kujivunia na kulinda uzuri wa mazingira asilia na kuhamasishana kuyatunza na kuhifadhi huku akiwaasa wananchi kuepuka madalali wa mkaa ambao kwa maelezo yake hufika katani hapo na kuhamasisha shughuli za ukataji wa mkaa ambao kwa maelezo yake mkaa huo unanunuliwa kwa kiasi cha Tsh. 3,000 na kwenda kuuzwa kwa zaidi ya Tsh. 30,000 huko Bukoba jambo alilolitaja kama linachangia hali ya umaskini wilayani Karagwe.

Aliendelea kusisitiza kuwa Serikali wilayani humu imeamua kuhamasisha utunzaji wa mazingira wakati nchi yetu inapoelekea kwenye hatua ya kukuza maendeleo ya viwanda hapa nchini ambapo Wananchi wa Tanzania wanahimizwa kutunza mazingira hasa nchi yetu inapoingia kwenye kipindi hiki cha mageuzi ya viwanda kwani viwanda hivyo vinavyotarajiwa kuanzishwa vinategemea sana maliasili na mazao mbalimbali katika kuzalisha na kujiendesha.

Kwa upande, Kaimu Mkuu wa Iadara ya Usafi na Mazingira, Godwini Bana kupitia hotuba aliyoisoma kwa kwa mgeni rasmi, alibainisha kuwa Dunia kwa sasa inakabiliwa na changamoto ya uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi chanzo kikubwa cha tatizo hili kikiwa ni shughuli za kibinadamu huku katika nchi zilizoendelea, uchafuzi huu ukitokana na shughuli za viwandani, hususani uzalishaji na matumizi ya nishati itokanayo na makaa ya mawe na mafuta, wakati nchi zinazoendelea, tatizo hili linachangiwa na; uharibifu wa misitu; uzalishaji na utupaji taka hovyo; kilimo na ufugaji usiozingatia kanuni za uhifadhi;

makazi holela; uchimbaji wa madini; ukosefu ama kutokufuata mipango ya matumizi bora ya ardhi pamoja na shughuli za viwandani.

"Mojawapo ya matokeo ya shughuli hizi ni kuongezeka kwa gesi joto ambalo limepelekea pamoja na mambo mengine, mabadiliko ya misimu ya mvua; ukame; mafuriko; ongezeko la wadudu waharibufu (wa mazao na magonjwa ya binadamu ama mifugo); kuongezeka ama kupungua kwa kina cha maji ya bahari, maziwa, mito na mabwawa; uharibifu wa vyanzo vya maji; upotevu wa makazi ya viumbehai n.k." alisema Bw. Bana kupita hotuba hiyo.

"Sote tunafahamu kwamba zipo nchi hapa duniani zilizoharakisha maendeleo ya viwanda bila kuzingatia kanuni za uhifadhi wa mazingira na leo tunaona jinsi ambavyo wanahangaika kusafisha kwa gharama kubwa hewa na majiyaliyochafuliwa. Tunashuhudia katika nchi hizo kwamba kuna nyakati shule zinafungwa, Maduka na Ofisi zinafungwa na wananchi wanarazimishwa kutotoka nje ya nyumba zao ama kufunika pua na midomo yao kwa sababu hewa imechafuka kupita kiasi kutokana na moshi wa viwandani. Kwa kuwa tumeona gharama hiyo kubwa ya uchafuzi wa mazingira, ni muhimu sisi tukajifunza na kutofanya makosa waliyoyafanya wenzetu", aliendelea kusema.

Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani yaliamuliwa na Baraza la Umoja wa Mataifa la mwaka 1972,wakati wa Mkutano wa kwanza wa Umoja wa Mataifa uliohusu Mazingira huko Stockholm, nchini Sweden. Aidha, Azimio la kuunda Shirika la Umoja wa Mataifa la kushughulikia Mazingira Duniani, yaani United Nations Environment Programme (UNEP) lilipitishwa pia siku hiyo. Tangu wakati huo, nchi mbalimbali duniani zimekuwa zikiadhimisha Siku ya Mazingira Duniani kila mwaka tarehe 5 Juni, kwa ujumbe maalumu unaotolewa na Umoja wa Mataifa.



**Kaimu Mkurugenzi Mtendaji Wilaya, Bi. Ashura Kajuna(wa pili kushoto) akifurahi jambo wakati wanafunzi wa Shule ya Msingi Omkakajinja walipotumbuiza kwa shairi kwenye maadhimisho ya siku ya Mazingiza yaliyofanyika katika Shule ya Msingi hiyo hivi Karibuni.**